


FAHAMU MAMBO MUHIMU KUHUSU UGONJWA WA CORONA (COVID-19)

► COVID-19 ni nini?

COVID-19 ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na virusi jamii ya Corona.

► Corona ni jamii kubwa ya virusi vinavyosababisha maradhi kwenye njia ya upumuaji wa binadamu.

Maambukizi ya virusi vya Corona huenezwa kuitia majimaji yatokayo katika njia ya hewa pale mgonjwa anapokohoa au kupiga chafya, kugusa nguo au maeneo yaliyoguswa na mgonjwa wa Corona



Dalili za ugonjwa wa CORONA ni ;

- Homa
- Mafua
- Kupiga chafya
- Kikohozi kikavu
- Kuumwa kichwa
- Vidonda vya koo
- Mwili kuchoka
- Ugumu wa kupumua

Uonapo dalili za maambukizi ya Ugonjwa wa Corona (Covid-19) wahi katika kituo cha afya au piga 199 bure kwa maelezo.



Safisha mikono yako
mara kwa mara kwa maji
tiririka na sabuni au kwa
dawa ya kutakasa mikono



Epuka kusalimiana
kwa kushikana mikono



Funiki mdomo na pua
wakati wa kukohoza au
kupiga chafya



Epuka kugusa macho,
pua au mdomo



Kaa mbali angalau mita 1
au 2 na mtu mwenye homa
au kikohozi mwenye historia
ya kusafiri maeneo yenye
ugonjwa huu



Epuka
misongamano